

# Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
**Volume: 04 Issue: 01 | December-2025**

EAJK


# Uchunguzi wa Kiplato Kuhusu Udhibiti wa Maadili Katika Miziki Miwili ya Kisasa Nchini Kenya (*Seti na Stick*)


**Author**
**James Mwangi**
**Author's email:** jamwamu09@yahoo.com

**Masai Mara University, Kenya**



**Cite this article in APA**
Mwangi, J. (2025). Uchunguzi wa kiplato kuhusu udhibiti wa maadili katika miziki miwili ya kisasa nchini Kenya (Seti na Stick). *Eastern Africa journal of Kiswahili, 4*(1), 89-98. https://doi.org/10.51317/eajk.v4i1.872

OPEN ACCESS
A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 2025-10-13
Accepted: 2025-11-15
Published: 2025-12-18

Scan this QR to read the paper online



**Copyright:** ©2025 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).



**Ikisiri**

Utafiti huu ulichunguza umuhimu wa maoni ya mwanafalsafa Plato kuhusu fasihi. Nafasi ya maoni yake katika kudhibiti maadili kwenye miziki miwili katika nchi ya Kenya kwa ajili ya utovu wa maadili iliangaziwa. Miziki hii ni: *Seti* wa Bahati na *Stick* wa Khaligraph Jones. Licha ya mkazo uliowekwa wa kitamaduni na mila pamoja na kidini katika nchi ya Kenya kuhusiana na maadili, kungali kuna miziki ya kisasa inayokweza utovu wa maadili. Miziki hii iliibua mihemko na chachawizo kutoka kwa watu wengi kwa ajili ya maudhui yaliyopo, walakini kudhibitiwa kwayo na serikali kungali kuna utata. Madhumuni ya utafiti yalikuwa kutathmini ikiwa miziki hii ilifaa kudhibitiwa kwa kupigwa marufuku kwa ajili ya kukiuka maadili katika maudhui yake kwa kutumia msimamo wa Plato kuhusiana na dhima za fasihi na kubaini mbinu za kimtindo kwenye miziki hii. Nadharia ya Sanaa ya Kimaadili ya Plato ilitumika kwenye utafiti huku mihimili yake ikihusishwa miongoni mwa madhumuni. Utafiti huu ni wa kithamano na ulitumia muundo wa kimaelezo kuchanganua na kuiwasilisha data. Data ilipakuliwa kwenye mtandao wa *YouTube* kisha picha na maneno kwenye miziki hii yakachanganuliwa. Usampulishaji ulikuwa wa kimakusudi kwa kuteua miziki miwili iliyokuwa imeibua malalamiko mengi kutoka kwa umma. Matokeo ya utafiti huu yanabaini kuwa miziki hii inasisimua hisia za kingono, ina uchafu mwingi, husababisha utovu wa maadili na kufisidi akili za hadhira kwa njia ambayo Plato angepinga. Hivyo, inasababisha mijadala ya udhibiti wa maudhui ya miziki hii ya kisasa nchini Kenya. Ilibainika pia kuwa miziki hii imetumia anaphora, kuhamisha ndimi, jazanda, udamisi, usafidi, kinaya, ritifaa na misimu ili kurahisisha uwasilishaji wa maudhui. Utafiti huu unatoa mchango madhubuti katika ukosoaji wa fasihi yoyote ile kwa kuhusisha falsafa za kikale katika kuchambua fasihi za kisasa. Matokeo ya utafiti ni tija kwa wasomi wa fasihi, wahakiki wa masuala ya maadili, wasanii pamoja na Shirika la kudhibiti filamu na muziki nchini Kenya.



**Maneno muhimu:** *Gengetone, HipHop,* maadili, miziki, Sheng, udhibiti.

**UTANGULIZI**

Ingawa kuna uhuru wa wasanii na utungaji wa miziki katika nchi ya Kenya, kumekuwa na lalama nyingi kutoka kwa wananchi kuhusiana na ongezeko la utovu wa maadili. Miziki imekuwa nyenzo muhimu sana katika mawasiliano, burudani, kuliwaza, kutakasa nafsi, kitega uchumi, kufundisha na kupitisha maadili kwa walengwa. Miziki huwa na athari kubwa kwa hadhira inayotazama au kusikiliza kwa njia hasi na chanya. Huweza kupitisha maadili na kuwabadilisha watu kwa njia nzuri au kufisidi maadili. Miziki katika nchi ya Kenya imekuwa na nafasi kubwa sana katika kushawishi na kuathiri tabia za vijana. Miziki hii ya kisasa ya vijana imeathiriwa na mchanganyiko wa tamaduni za kigeni kama vile *Hip-hop*, *Afrobeat* na *Gengetone* ambayo mara nyingi hushughulikia maudhui ya mapenzi na mahaba.

Maudhui ya mapenzi, ngono, uasi na dawa za kulevya hushabikiwa na kuvutia hadhira kubwa ya vijana. Kusambazwa kwa miziki kumewezekana sana kwa ajili ya ukuaji wa teknolojia ya kisasa kama vile matumizi ya simu tamba, tarakilishi, santuri, tepurekoda, kamera za kisasa na video. Miziki mingi huwasilisha maudhui kwa njia ya moja kwa moja pasipo kutumia mafumbo na tasfida hata pale ambapo inahitajika. Kutokana na haya, imesababisha upotoshi kwa hadhira lengwa kwa ajili ya kukosa kudhibitiwa. Hali ya kudhibiti maadili katika jamii ni suala ambalo limezua mijadala ya kifalsafa miongoni mwa watu katika nchi mbalimbali huku maoni ya Plato kuhusiana na fasihi yakiwa na mchango kabambe katika ulindaji wa maadili katika jamii. Udhibiti wa awali kabisa wa muziki ulishuhudiwa mwaka wa 1735, ambapo mchapishaji John Peter Zenger alikabiliwa na shinikizo la kisheria kwa ajili ya kuchapisha maneno ya wimbo mmoja uliokuwa umekashifu na kukosoa serikali ya Uingereza.

Katika nchi ya Kenya, miziki ya kisasa imekabiliwa na matatizo chungu nzima kama vile kukosekana kwa sheria madhubuti za kudhibiti maudhui yaliyomo ya kidijitali na athari za utandarihi ambao huimarisha maudhui ya kigeni dhidi ya yale ya kienyeji. Hali ya kudhibiti fasihi kama vile miziki na filamu ni suala la kidunia ambalo halijafungiwa macho na watu. Kudhibiti miziki kulijitokeza sana katika miaka ya 1950 na 1960 kwa ajili ya hofu ya kuchipuka kwa mitindo ya R&B ambayo ilifurahiwa na kushabikiwa na watu wa Marekani wenye asili ya Afrika na iliitwa "miziki ya kishetani" (Stone, 2022). Snapes (2019) aliweza kujumuisha nyimbo ishirini zilizotungwa kwanzia 1965 hadi 2013 akizifafanua kama 'nyimbo ambazo zimewahi kupigwa marufuku za wakati huo,' nyimbo hizi alizifafanua kama zilizo na lugha chafu na zinazoshughulikia sherehe za kilevi ambazo zilikuwa zimefisidiwa na hazikufaa kuruhusiwa kusikilizwa na watu.

Katika nchi ya Kenya, aliyekuwa msimamizi wa Shirika la kudhibiti filamu na muziki nchini Kenya, Ezekiel Mutua alijitokeza kwa uwazi na kupinga miziki iliyokuwa na maudhui machafu ambayo pia yalikwenda kinyume na misingi ya kimaadili ya nchi. Upigwaji marufuku wa miziki iliyokiuka maadili katika nchi ya Kenya ulikuwa umefanyika kati ya mwaka wa 2018 na 2023. Nyimbo saba za *Gengetone* zilizokuwa zimesheheni utovu wa nidhamu kwa kutumia lugha chafu ziliathirika wakati huo.

Kutokana na ukuaji wa sanaa katika nchi ya Kenya pamoja na uhuru ulioko, hali ya upujufu imeshuhudiwa. Suala hili limesababisha wasiwasi na kusababisha uchunguzi wa miziki miwili ya kisasa katika nchi ya Kenya. Nayo ni: *Seti* (2025) uliotungwa na Bahati ambaye alikuwa mwimbaji wa nyimbo za kidini kabla ya kuingilia miziki mingine isiyo ya kidini na *Stick* (2024) uliotungwa na Khaligraph Jones ambaye ni maarufu katika nyimbo za *HipHop.* Utafiti huu ulihakiki ikiwa maudhui yanazingatia maadili kwa kutumia kigezo cha Kiplato kuhusu fasihi. Pia ulibaini ikiwa udhibiti wa maadili ulifaa ili kuzuia upotoshi kwa hadhira lengwa.

Utafiti wa kutosha kuhusu athari za maudhui ya miziki ya kisasa na mbinu za kudhibiti maadili una mapungufu. Hivyo, kuna hatari ya kuendeleza migogoro ya kimaadili na kuharibu maadili ya kitamaduni na mila zenye thamani katika nchi ya Kenya. Utafiti huu unaziba pengo hili kwa kuchanganua maudhui ya miziki hii miwili na mbinu za kimtindo zinazotumika katika uwasilishaji wa ujumbe. Unapendekeza ikiwa inafaa kudhibitiwa kwa kutumia misingi ya Kiplato kuhusu ubora wa Fasihi. Unanuia kutoa maarifa ya kinadharia ya namna miziki maarufu ya Kenya inaweza kudhibitiwa na Shirika la kudhibiti Filamu na Muziki nchini Kenya bila kukandamiza uhuru wa kisanii. Pia unaweka kwa uwazi kuwa udhibiti wa maadili katika nchi ya Kenya unafaa kufanya kazi kwa

uzingativu wa maoni ya Plato kuhusu sanaa na fasihi kwa ajili ya kulinda maadili na tamaduni za jamii.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Mutua (2019) anadai kuwa miziki ya aina ya Gengetone ni uasi wa kitamaduni, maadili ya jamii, dini na Mungu. Kulingana na maoni yake, aina hii ya miziki huwa inafaa kuchunguzwa sana ili kuchunga yaliyo machafu kwa ajili ya hadhira lengwa. Anasema kuwa miziki inaweza kuathiri msingi wa kimaadili wa nchi ikiwa haitadhibitiwa. Maoni haya ni muhimu kwenye utafiti huu kwa kuwa yanaonyesha umuhimu wa kuchunguza miziki ya kileo ya vijana ili kuondoa yanayoweza kuvuruga jamii kimaadili. Hii inaashiria kuwa miziki ya vijana wa kisasa huwa imebeba maudhui ambayo hukinzana na maadili hivyo ni muhimu kutiliwa maanani kabla ya kusambazwa kwa hadhira.

Mutua (2021) anasema kuwa miziki ya aina ya Gengetone hubeba maneno na picha ambazo huendeleza uovu kama vile matumizi ya dawa za kulevya na kushabikia mno unajisi wa jinsia za kike. Haya kwa hivyo husababisha maovu ya kiakili. Maoni haya ni muhimu kwenye utafiti kwa kuwa yanaonyesha maudhui yaliyo kwenye miziki hii ya Gengetone, ambayo hushabikiwa mno na vijana. Yatasaidia utafiti huu kwa kuchunguza maudhui ambayo hayafai pamoja na picha zilizo hatari kwa kizazi cha sasa kwa ajili ya kudhibitiwa.

Kasyoka (2022) alifanya utafiti kuhusu maudhui yenye matatizo kwenye nyimbo za *Gengetone* katika nchi ya Kenya. Uchunguzi wake uliongozwa na nadharia ya Semiotiki. Utafiti wake ulionyesha kuwa nyimbo za *Gengetone* zilibeba maudhui kama vile ukosefu wa uaminifu, mashambulizi, kutotiii, kutojizuia, ufuska na matumizi ya dawa za kulevya. Utafiti wake ni muhimu kwenye utafiti huu kwa kuonyesha kuwa baadhi ya miziki ya vijana wa kileo huwa na maudhui ambayo hufaa kuangaliwa kwa macho ya upekuzi ili kuondoa yasiyostahili. Utasaidia utafiti huu kimaoni kwa sababu unashughulikia miziki ya aina moja ya vijana. Tofauti ni kuwa miziki iliyoshughulikiwa awali ni ya 2021 na mitindo hubadilika kila mara kwa ajili ya mpito wa wakati. Utafiti huu ulitumia nadharia ya Sanaa ya Maadili tofauti na wa awali.

Muchunku (2023) alitafiti kuhusu utaratibu unaochukuliwa katika kudhibiti nyimbo katika Afrika Mashariki kwa kujikita katika nchi mbili-Kenya na Tanzania. Utafiti wake ulibaini kuwa kati ya 2018 na 2023 nyimbo ishirini za Bongo Flavas kutoka nchi ya Tanzania na saba za Gengetones zilipigwa marufuku kwa ajili ya kwenda kinyume na mila na tamaduni za jamii, hivyo kuhakikiwa kuwa ni mbaya kwa watoto na wananchi katika kanda hii. Utafiti wake ni muhimu katika kuujenga utafiti huu kimawazo kwa kuweka wazi yale yanayoweza kusababishwa miziki kudhibitiwa.

Ndiritu et al. (2024) walibainisha hatua za udhibiti wa matangazo ya televisheni katika nchi ya Kenya unaotekelezwa na shirika la kudhibiti filamu na miziki. Utafiti wao ulidhihirisha kuwa udhibiti na uzuiliaji wa matangazo kwenye runinga huchochewa mno na kuwepo kwa maudhui ya kingono yanayokosa maadili. Kadhalika, udhibiti huchochewa na haja za kulinda watoto pamoja na vijana kutokana na kuiga tabia ambazo hazistahili. Utafiti wao japokuwa ulilenga matangazo kwenye runinga, ni faafu kwa utafiti huu kwa kuonyesha kichocheacho udhibiti wa sanaa pamoja na aina za maudhui ambayo husababisha kudhibitiwa kwa kazi ya sanaa kama vile miziki.

adelaja oriade, (2020) alibaini kuwa kuna matumizi ya mbinu za kimtindo kwenye nyimbo za *Hip-Hop* katika taifa la Nigeria hasa zile ambazo zinaendeleza chuki kwa wanawake. Alidhihirisha kuwa nyimbo nyingi za *Hip-Hop* hutumia lugha inayoendeleza chuki kwa wanawake na kuwafanya wanawake kama vifaa kwa ajili ya kutosheleza ashiki za wanaume hivyo basi ni kinyume katika ukuzaji wa jamii yenye haki. Maoni yake yaliufaa utafiti huu kimawazo kwa kuonyesha mbinu za kimtindo ambazo hutumiwa kwenye miziki ili kuwasilisha maana na baadhi ya maovu ambayo hupatikana kwenye nyimbo nyingi za *Hip-Hop*.

Tafiti hizi za awali ni muhimu kwenye utafiti huu kwa kuweka misingi ya kimawazo hasa kuhusiana na miziki ya vijana wa kileo. Pamoja na hayo inaonyesha jumbe mbalimbali ambazo huwa zimesheheni kwenye miziki hii. Tafiti hizi zinaonyesha kuwa miziki mingi ya vijana huwa na maudhui ambayo huibua mihemko kwa hivyo huhitaji kuchunguzwa kwa umakinifu.

**Msingi wa Nadharia**

Nadharia ya Sanaa ya Kimaadili ndiyo ilikuwa msingi kwenye utafiti huu. Ilibuniwa Ugiriki na mwanafalsafa

Plato (427-347 KK) kisha ikaendelezwa na Aristotle. Ilizuka wakati ambao sanaa hasa ushairi, drama, na miziki ilikuwa na athari kubwa katika kujenga maadili na tabia za wananchi wa Kigiriki. Kulingana na Wagiriki, waliona sanaa si kama burudani pekee bali ilikuwa taasisi yenye nguvu ya kijamii ya kulinda maadili. Plato alikuwa mwasisi na mtu mwenye athari kubwa wa kimaadili. katika kazi zake hasa The Republic, Ion na The Law alidai kuwa sana hasa ushairi na drama zilifaa kuwa na maadili na mafundisho. Kulingana naye, sanaa ilikuwa shughuli za wigo ambazo zingekweza na kufisidi nafsi. Aliamini kwamba wasanii huwa wanaiga mwonekano lakini si ukweli hivyo kazi zao zinaweza kuathiri hisia na kuwafanya watu kukosa kutumia akili, kuwa na urazini na tabia nzuri. Kwa hivyo, sanaa ilifaa kudhibitiwa ili kuhakikisha kuwa inaendeleza wema na utaratibu.

Baadaye, Aristotle (384-322 KK) alichukua usukani na kupinga maoni ya Plato kuhusiana na kudhibitiwa kwa fasihi. Yeye alikubali nguvu za kimaadili za sanaa na Fasihi. Alidai kuwa tanzia hufanya hadhira kuondoa hisia kama vile huruma na woga na kusababisha usawazishaji wa maadili na hisia. Kwake, sanaa na fasihi zilikuwa na dhima za kimaadili na kisaikolojia si kwa ukandamizaji bali kwa mafunzo ya kihisia. Horace naye aliamini kuwa sanaa yafaa kufunza na kufurahisha. Haya yaliathiri wanafalsafa wa Kikristo huku wakidai kwamba sanaa yafaa kumtukuza Mungu na kuendeleza wema. Kanisa nalo lilidhibiti sanaa huku likisisitiza kuwa sanaa yafaa kufanya kazi ya kidini na kimaadili. Katika kipindi cha mwamko, sanaa ilianza kufurahiwa kwa ajili ya ulimbwende huku maadili yakiwa mhimili mkuu. Katika karne ya ishirini mikabala ya kimaadili iliendelea katika uhakiki wa kifasihi hasa katika uhalisia wa kijamii na sanaa ya kimaadili.

Utafiti huu ulitumia mihimili ya nadharia ya sanaa ya kimaadili kama ilivyopendekezwa na Plato ikiwemo: fasihi huwa na athari mbaya kwa hadhira, fasihi huathiri maadili kwa njia ya kupotosha hadhira, fasihi ni wigo wa uhalisia kwa hivyo ni uongo, fasihi huathiri hisia na udhibiti wa fasihi (kuwa serikali ina jukumu la kudhibiti sanaa ambazo zinahatarisha maadili). Plato katika kitabu chake maarufu, *The Republic X,* alijiundia Jamhuri yake ya kisanaa ambapo alidadavua umuhimu wa kufutilia mbali fasihi. Alipendekeza fasihi ipigwe marufuku kwa kudai kwamba ilikuwa na mchango mkubwa katika kuubeba uongo badala ya kuwa na ukweli. Alisema kuwa mtunzi wa kazi ya fasihi kwa ajili ya ubunifu alikuwa na uwezo wa kuwasilisha mambo yaliyo ghushi na kuyafanya kuwa ya kweli. Kadhalika, alisema kuwa mtunzi huhusisha mwigo wa vitu visivyofaa kuwepo na kujifanya kuwa anavielewa. Kadhalika, alisema kuwa fasihi ilifaa iendeleze haki na maadili kwa watu. Hivyo alidhibiti fasihi ambayo ingechangia kufisidi akili na kuchochea uovu.

Kulingana naye, fasihi ilikuwa na mchango katika utovu wa nidhamu kwenye maisha ya watu. Alipendekeza ufutiliaji mbali wa fasihi kwa kusema kuwa; hisia na burudani zilipewa nafasi kubwa katika maisha ya mwanadamu na kupuuza matumizi ya akili. Vilevile, alipinga uchangamfu uletwao na fasihi na hisia zinazoibuliwa kiasi cha kujisahau hivyo akapendekeza akili na urazini ziwe kipaumbele. Aliona pia kuna mchango mkubwa hasi wa fasihi katika maisha ya watu (hadhira) kwa kuwaathiri vibaya kama vile kuwaliza watu mahali ambapo wanafaa kuburudika, kuwachekesha mahali ambapo wanafaa kulia na utendaji wa mambo ya fedheha kwa mwiigizaji (fanani) ambapo kiuhalisia hangetenda vile. Haya aliyachukulia kama usaliti wa nafsi ya mtu. Vilevile, alichukulia fasihi kama wigo ambao ulifumba uongo na ulipotosha. Mihimili hii yote iliyotajwa ilitumika katika utafiti huu.

**MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti huu ni wa kithamano na ulitumia muundo wa kimaelezo uliojihusisha katika kuchanganua suala la utafiti pasi na kubadili vibadala. Muundo huu ni mwafaka kwa sababu unaweza kutumika kukusanya data kuhusiana na maoni ya watu, kuhusiana na suala fulani, hisia za watu, tabia, au aina nyingine yoyote ya masuala ya kijamii (Orodho & Kombo, 2002). Mtafiti alisaidika kwa kuangalia maoni ya watu kupitia usomaji kwenye mitandao, kueleza na kunukuu yaliyosemwa bila kubadili chochote. Eneo la utafiti lilikuwa mtandaoni kisha tasnifu na kazi zinazohusiana na mada zikasomwa kwenye maktaba ili kujaza na kurutubisha kazi ya mtafiti. Data ilikusanywa kupitia upakuaji kutoka kwenye mtandao wa *YouTube* kuhusu nyimbo mbili teule kisha zikasikilizwa na kutazamwa kwa makini na mtafiti halafu mbinu za upekuzi-changanuzi zikatumiwa kufafanua yaliyokuwepo. Uteuzi wa sampuli ulikuwa wa kimakusudi ambapo nyimbo mbili zilizokuwa zimesababisha malalamiko kutoka kwa hadhira zilivutia umakini wa mtafiti. Nyimbo hizo ni *Seti* na *Stick* za Bahati na Khaligraph



DRAFT

Jones. Uchanganuzi wa data hii ulifanyika kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya Sanaa ya Kimaadili huku malengo ya utafiti yakizingatiwa.

**MATOKEO YA UTAFITI**

**Maudhui**

Wimbo huu wenye anwani *Stick,* umeimbwa na Khaligragh Jones kwa anayeonekana kuwa mpenzi wake huku akionesha hisia za mapenzi na kutaka kujamiana naye.

> *Baby, you know I'm out here working. I know you miss me, but I miss you too. I'm coming back home pretty soon. I'm out here just trying to put in that good work. As soon as I am done, nakuja mtaa so wait for me. Meanwhile, gotta message for you, just listen. Nakuja kukupiga stick nakuja kukupiga miti. I know you've been yearning for this uu saa imeshapita kawiki najua. Kuna vile unanimiss. Usijali mambo itakuwa fiti, nakuja kukupiga kiss. Nakuja kuguza mati. Nakuja kukuchapa kwa kiti. As soon as I land in the city. Hiyo sikuwa sivai hata panty juu nakuja na njia ya fisi. As soon as umefika Nairobi airport ntakupiga kaquickie, then as soon as tufike kwa keja. I swear utajua ni mazishi. I'm coming to give you the tongue coz baby you know you de one. I am coming to lick it, and girl, I am a lick and lick it until I am done. Nimekua na mafantasies. Can't wait till nipande hiyo ndege. Nimechoka kupigwa njeve. Nakuja kukupunguzia nyege. Huku statoe madem ni kibao wananitamani mpaka walami, wananioffer punani but mi nataka ile nmeacha nyumbani. Nakuja tumisbehave kaa zile parky za Masaku juu si wawili tuwachani kama Mathenge na Wahu. Sijali mnaisema hadharani. You a queen si msichana flani. Na pia naona ukiwa mama nani juu nakuja kaa nimemwaga ndan*.*

Mwimbaji ambaye ni mwanamume anatanguliza kwa kusema kuwa yuko nje akifanya kazi na kumhakikishia mpenziwe kuwa atarejea ili wawe pamoja. Anaeleza jinsi alivyompeza mpenzi wake. Hii inaashiria uhusiano wa karibu ambao una vizingiti kwa ajili ya umbali. Baadaye anamhakikishia kuwa lazima atafika kwa hivyo aweze kumsubiri. Anampa hakikisho kuwa afikapo ni lazima atashiriki naye mapenzi. Anaonyesha uhusiano wa karibu wa hawa wawili kiasi cha kushiriki mapenzi. Mwanamume anaonyesha jinsi uchu wa kufanya mapenzi unavyomchochea kufika nyumbani. Kadhalika, anatumia maneno ya ushawishi ili kusisimua hisia za mpenziwe kwa kusema kuwa, *nakuja kukupiga kiss, nakuja kuguza mati, nakuja na kukuchapa kwa kiti*. Haya yote yanaashiria tamaa kubwa ya mapenzi huku akionyesha bila kuficha wala kuwa na tasfida. Maudhui ya mapenzi yaliyojengwa kwa misingi ya ashiki ya ngono yanadhihirika.

Anatumia lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa nia ya kunasa kizazi cha vijana ambacho ndicho hushabikia miziki na mitindo hii ya uimbaji pamoja na kusawiri uhalisia wa yale anayoyasimulia. Zaidi, mwimbaji anasema kuwa *sikuwa sivai hata panty juu nakuja na njia ya fisi*. Maneno haya yanaashiria uchi na urejelezi wa fisi yanaonyesha atakavyofika kwa pupa, sawa na alivyo fisi. Atafika akiwa na hamu ya kufanya mapenzi. Anaendelea kwa kudai kuwa *nitakupiga kaquickie utajua ni mazishi* huku akiashiria kujamiana kwa fujo. Baadaye, anasema *Am coming to give you tongue coz baby you know de one.* Anaelezea waziwazi tendo la maandalizi kabla ya kushiriki ngono bila kuficha. Anamalizia kwa kudai kwamba, *you a queen si msichana flani nakuja kaa nimemwa* nda*.* Hapa amsifu mrejelewa na kukiri kwamba yu tayari kushiriki kitendo cha ngono bila kinga ili aweze kumtunga mimba apate kuitwa mama ya fulani.

Vilevile, usodai na majishauo katika tendo la ngono yanajengwa na mwimbaji. Anakiri kwamba *I swear utajua ni mazishi.* Haya yanadhihirisha jinsia atakavyotekeleza lile tendo. Kutengana kwa muda mrefu kwa wapenzi hawa kunasababisha kupezana. Mwimbaji anadhihirisha jinsi atakavyofurahia katika tendo la kujamiana punde tu atakapowasili. Uunganisho wa kihisia unajitokeza kwenye wimbo kati ya mwimbaji na mpenziwe. Anathibitisha kuwepo kwa utengano kwa sababu ya mtindo wake wenye majukumu mengi ya kikazi. Anasema, *baby you know I am out here working, I know you miss me, and I miss you too*. Maneno haya yanaonyesha mapenzi ya dhati yenye uaminifu ijapokuwa yamekumbwa na utengano anapokiri kuwa, *I must put that good work.* Haya yanamsawiri kama mchapakazi anayeweza kutegemewa na mpenziwe.

Kutokana na maoni ya Plato, fasihi inafaa ikuze wema. Hata hivyo, wimbo huu umejengeka kwa uchu wa ngono kwa kuzingatia yale ambayo mwimbaji



DRAFT


anayakiri. Kibwagizo cha wimbo huu ni kuwa *nakuja kukupiga sti* na nakuja kukuguza mati**. Wimbo huu unakiuka wema na maadili. Kulingana na maoni ya Plato, fasihi ilisukuma watu kusisimka kihisia na hivyo kuwatenga na ukweli halisi kama ilivyo kwenye wimbo huu. Mwimbaji anasisimua hisi za kimapenzi na kuna uwezekano akazuga akili za hadhira kwa maneno aliyoyatumia. Kutokana na haya, aina hii ya fasihi haifai kabisa kwa hivyo inafaa idhibitiwe au kupigwa marufuku hasa kwa vijana na watoto wachanga.

Plato alipendekeza udhibiti wa fasihi kwa kuwa ni wigo na wakati mwingine huiga matendo mabaya au matendo yasiyodhihirisha maadili. Msanii huyu kuzungumzia vitendo vya ngono waziwazi pasi na kutumia tasfida ni utovu wa maadili. Pia, kuzama sana kwenye vitendo vya ngono vitasisimua nafsi na kuzuia urazini. Alichokiangazia mno kuanzia mwanzo hadi mwisho ni tendo la kujamiana hivyo hakuna uhalisia wowote. Katika ubunifu huu, mwimbaji anaonyesha utovu wa maadili kwa kusema kinaganaga masuala ya kujamiana ambayo ni mwiko kulingana na tamaduni za jamii nyingi nchini Kenya na hayaruhusiwi kusemwa kwa uwazi. Plato alisema kuwa fasihi ya aina hii ilifaa kuepushiwa watoto wasije wakapotoka kimaadili. Vilevile, kuna uwezekano itaacha athari mbaya kwa vijana ambao ndio walengwa hivyo yafaa kupigwa marufuku.

Katika wimbo wa pili ulioimbwa na Bahati una mtiririko ufuatao:

> *Anasema eti nimpe pesa atanionjesha na hatanisema kwa mamaz, ila simwamini, simwamini, ila simwamini, simwamini. Kama last time ulinipea kiss na ukaniseti, hivi nikikupea doo utaiseti? Mimi ni player nadai ball ndani ya net, mtoto m-fine mtoto cute, mtoto keki, seti (uuuuh, auuuuh set). Usinyime si sabuni eti itaisha, usininyime nitaigonga, usininyime si unasema eti unasema umeokoka, usininyime uchi wa dhambi. We ni m-fine we ni m-cute mtoto keki.*

Wimbo Seti, anwani yake ni tasfida iliyotumika kumaanisha siri au hali ya kukutana. Umetumia lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng (ambayo ni lugha ya mitaani inayozungumzwa sana na vijana katika nchi ya Kenya). Maudhui makuu yanayoshughulikiwa ni utongozaji unaoandamana na mahusiano ya kimapenzi sawa na ilivyo kwenye wimbo wa Khaligraph Jones. Katika utangulizi mwimbaji anadai kuwa mrejelewa anayeonekana kuwa mwanamke anaomba pesa ili aweze kukubali kushiriki naye mapenzi. *Seti*, umetawaliwa na lugha ya kingono na yenye kuvutia hisia za mapenzi. Mtazamaji anapozitazama picha na video kwa mara ya kwanza anafahamu kwa uwazi kinachoangaziwa na wimbo huu. Picha hii ni mfano mzuri wa upujufu unavyojitokeza katika wimbo mzima.



**Kielelezo 1: Picha kutoka video rasmi ya muziki ya Seti na Bahati**

Yanayodhihirika katika ubeti wa kwanza ni ushawishi, kutoaminiana na ubidhaishaji wa mapenzi kwa sababu 'mwanamke' anaomba pesa kwanza kabla ya kuitikia kujiingiza katika tendo la ngono. Ijapokuwa mwanamke anatoa ahadi kwa mwanamume ambaye ndiye mwimbaji, mwanamume anasema kuwa hamwamini. Maudhui ya ukosefu wa uaminifu yanakuzwa. Anasisitiza kuwa hamwamini kwa kuwa

DRAFT

mara ya mwisho alipokubali kumpiga busu alikosa kuweka siri. Yanayodhihirika kwa uwazi ni mahusiano ya siri ya watu wawili ambao hawaaminiani huku mmoja akihofia kusalitiwa na mwenzake. Wimbo unaonyesha uhalisia wa mahusiano miongoni mwa vijana wa kisasa.

Kadhalika, mwimbaji anaonyesha hamu yake ya kutaka kushiriki mapenzi anapomwambia kwamba yeye ni *player anayedai ball ndani ya neti*, ametumia tasfida inayomaanisha kuwa na uzoefu na ushindani katika tendo la kujamiana. Anaendelea kutoa sifa tele za mpenzi wake kama njia ya kumrai huku uzuri wake ukilinganishwa na keki. Mwimbaji anamsihi mrejelewa kuwa asikatae kushiriki naye mapenzi huku akimwarifu kuwa uke wake sio kama sabuni ambayo huisha. Tendo la jimai linafanywa kama biashara ambayo washiriki wawili hujadiliana bei kabla ya kuafikiana. Tamati ya wimbo huu ni kauli ya dhihaki kwa mwanamke kwa kudai kuwa ameokoka huku mwanamume akimwambia kuwa *ataigonga* (kujamiana naye kwa fujo) na asimnyime uchi wa dhambi. Kudai kuwa ni uchi wa dhambi ni kujaribu kuonyesha uhalali wa mwanamume kuingiliana na mwanamke huku akionyesha kuwa hapana makosa.

Maoni ya Plato kuhusu fasihi ni kwamba ni wigo. Kulingana naye, fasihi inasawiri na kutukuza uovu kwa kuiga matendo maovu. Mwimbaji wa wimbo anaiga "mchezaji" mdanganyifu ambaye anaomba kujamiana kwa kutoa pesa na anakosa kumwamini mwanamke. Plato anaonya kuwa wigo unazoesha nafsi na kupamba maovu sawa na inavyojitokeza katika wimbo huu. Kuna uwezekano hadhira ambayo ni vijana wataiga yale yote ambayo wanayasikiliza na kuona kwenye wimbo kama tendo la kujamiana. Hivyo haufai kukumbatiwa katika kizazi cha leo. Kadhalika, wimbo huu unachochea hisia na hamu za kujamiana. Yanayojitokeza katika wimbo mzima ni upaliliaji wa raha ya mapenzi bila kuhusisha urazini katika ushirikiano, hivyo unafaa udhibitiwe.

Wimbo huu vilevile una utovu wa maadili. Mwimbaji anazungumzia kitendo cha ngono kinagaubaga bila kutumia tasfida ilhali suala hili linafaa kuwa siri. Wimbo huu pia umehusisha picha chafu ya mwanamke na mwanamke wakiwa nusu uchi huku wakishiriki katika kubusiana na kulaliana. Ni mwiko na kinyume na utamaduni wa jamii za Kiafrika. Wimbo kama huu unafaa kuepushiwa watoto na vijana kwa kuwa unaweza kusababisha wao kuiga na kutenda wanayotazama na kusikiliza. Kwa misingi ya Plato, fasihi ya aina hii ni potovu na itavuruga akili za hadhira. Mwanamke na mwanamume kwenye picha hii wanaonyesha mmong'onyoko wao kwa njia isiyo ya staha kwa kupigana busu na kukaliana. Kitendo hiki kinaashiria upujufu utakaoacha athari hasi kwa hadhira.



**Kielelezo 2: Mwanamume na mwanamke wakipigana busu**

DRAFT

**MBINU ZA KIMTINDO**

**Uradidi/anafora**

Uradidi ni hali ya kurudiarudia neno fulani au sentensi. Hutumika sana kwa ajili ya kusisitiza ujumbe hasa katika kibwagizo na vilevile mfululizo wa wizani. Wamitila (2003) anasema kuwa anafora ni mbinu ya kibalagha au ya kiusemi ambayo huhusisha kurudia neno au kundi la maneno katika vishazi au sentensi zinazofuatana. Maneno *simwamini, seti, I miss you too, nakuja kukupiga sti**, nakuja kukupiga miti* yamerudiwarudiwa ili kusisitiza ujumbe, kutia nguvu ujumbe wa mwimbaji kwa kuonyesha hali ya kutomwamini mpenzi wake na kuonyesha kuteseka kwake kihisia. Pia kauli *nakuja* inaonyesha jinsi anavyotazamia kukutana na mpenzi wake ili ashiriki naye mapenzi. Wizani kwenye miziki inaweza kuvuruga hisia za hadhira na kuwafanya wapokeaji wa jumbe kupata yasiyokuwa na maadili. Hivyo, kulingana na maoni ya Plato, fasihi hii haifai.

**Kuchanganya ndimi/ kuhamisha ndimi na matumizi ya misimu**

Kuna hali ya kuchanganya lugha zaidi ya moja katika sentensi moja au kwenye matini. Lugha ya Kiingereza, Kiswahili na Sheng zimetumika katika miziki hii miwili kuonyesha uwezo wa kutumia lugha mbili wa mtu. *Baby you know I'm out there working, I know you miss me, but I miss you too… nakuja kukupiga sti** nakuja kukupiga miti.* Hii inaonyesha uwezo wa kumanya lugha nyingi miongoni mwa vijana wa mitaani na huakisi utamaduni wao wa mijini. Imetumika ili kuonyesha uhalisia na upekee wa waimbaji, wanayoyashabikia na pia kuwatenga watu wasiofaa kujua maudhui kwenye wimbo huu kama vile wazee.

**Jazanda/mafumbo**

Lugha fiche na ya kimafumbo imetumika katika miziki hii miwili ili kuficha ujumbe kwa wasiolengwa mathalan, kwenye wimbo wa *Seti,* mwimbaji ametumia kauli zifuatazo: *Mimi ni player nadai ball ndani ya neti*. Kujiita *player* au mchezaji ni kuonyesha uwezo wake wa kutekeleza tendo la ndoa. Kusema kuwa *anadai ball ndani ya neti* anamaanisha kuwa angetaka kushiriki mapenzi na mrejelewa japokuwa hataki kutumia lugha ya moja kwa moja. Anwani Seti pia imetumia kijazanda kuashiria kusalitiwa au kudanganywa ama kufanya mambo kisiri. Limetumika kuonyesha maudhui ya ulaghai katika mahusiano na kukosa kuaminiana. Katika lugha ya mtaani, kuseti ni kufanyia mtu ujanja hivyo imetumika kujenga ujumbe wa hila. Pia wimbo wa *Stick* mwimbaji ametumia lugha ya kimafumbo kwa kusema kwamba: *Nakuja kukupiga sti**.* Kwenye sentensi hii, anamaanisha kuwa anakuja kujamiana naye huku neno *stick* linalomaanisha kijiti likitumiwa kifumbo kusawiri dhakari na uwezo wake wa kuingilia mwanamke. Pia *kukuchapa kwa kiti* ni jazanda iyomaanisha kushiriki mapenzi huku wakiwa kwenye kiti tofauti na maana ya kawaida inayojulikana.

**Chuku/Udamisi**

Ni hali ya kutia chumvi kwenye sentensi au maneno ambayo mtu husema. Hukuza sifa ya kitu fulani zaidi kuliko kawaida yake. Wimbo wa *Seti* umetumia chuku kwa kumrejelea mwanamke kama *mtoto keki.* Inaeleza jinsi mwanamke mrejelewa alivyo mrembo hata analinganishwa na keki. Udamisi umetumika katika wimbo wa *Stick* huku mwimbaji akidai kuwa, *Huku statoe madem ni kibao wananitamani mpaka walami, wananioffer punani.* Anasema kwamba aliko katika nchi ya mbali anatamaniwa hata na Wazungu ili washiriki naye mapenzi lakini amekataa kwa kuwa anataka alichokiacha nyumbani. Haya maneno ni chuku huku yakimsawiri mwimbaji kama mtu mwaminifu sana kwa mpenziwe na kwamba amekosa kuwa na uhusiano hata na walio wazuri *walami* (Wazungu) kwa ajili yake. Haya ni maneno ya kumshawishi na kujenga taswira za kimapenzi, kuonyesha hali ya hisia na kuongeza matamanio.

**Tasfida/usafidi**

Hii ni tamathali ya usemi ambayo hutumia lugha ya staha au ya kificho badala ya kutumia moja kwa moja. Huzuia ukeraji wa wasomaji au wasikilizaji. Kwenye wimbo wa *Seti*, usafidi unadhihirika ifuatavyo: *"Nimpe pesa atanionjesha. Usininyime si sabuni. Usininyime uchi wa dhambi".* Mistari hii imetumia lugha fiche kwa kuficha makali ya kutaka kujamiana moja kwa moja. Inajenga hisia kwa kuepuka lugha chafu ambayo itaudhi wasikilizaji. Pia inatumiwa ili kuinasa hadhira ambayo ni vijana.

**Kinaya**

Tamathali hii ya usemi huonyesha mambo ambayo hufanyika kinyume na matarajio. Kinaya kinajitokeza ifuatavyo katika miziki hii miwili: *"Usininyime uchi wa dhambi, we unasema umeokoka."* Ni kinaya kwa mwanamume kumdhihaki mwanamke huku akitaka kushiriki naye mapenzi ilhali anafahamu na kudai kuwa

yeye ameokoka. Kwake anachukulia kuwa mwili wa mwanamke unafaa kutumika katika kujamiana bila kizuizi chochote. Hii inaashiria unafiki wa kidini ulioko kwa kuwa anayedaiwa kuwa ameokoka anajihusisha katika mahusiano ya kingono. *"I swear utajua ni mazish"* Kauli hii imetumika kwenye wimbo wa *Stick* mwimbaji akisema kuwa punde atakapowasili kwenye uwanja wa ndege, atajamiana naye haraka haraka na watakapoingia kwenye nyumba atajua kuwa ni mazishi. Hii inaashiria kuwa kitendo cha ngono kitafanywa kwa fujo. Ni kinaya kushiriki mapenzi ya aina hiyo kwa mtu unayempenda hata kulinganisha tendo hilo na mazishi ilhali linafaa kuleta burudani.

**Tashibihi**
Ni hali ya kulinganisha vitu viwili kwa kutumia maneno kama vile, kama, ja na mithili ya. Kwa mfano, mwimbaji wa wimbo wa *Stick* anasema kuwa, *"Kama Mathenge na Wahu, tumisbehave kaa zile parky za Masaku."* Maneno haya yanarejelea wasanii wawili (mume na mke) ambao ni tajika katika nchi Kenya na vilevile kulinganisha na sherehe za burudani za Machakos ambapo hutambulika kwa uhuru wa kushiriki ngono. Kuwataja Wahu na Nameless ni kuonyesha hali yao ya ushirikiano wa mapenzi kama wanandoa wawili walio waaminifu. Anamwonyesha mpenziwe kuwa watakuwa kama wasanii hawa wawili.

**Ritifaa**
Hii ni mbinu ambayo mtu humsemesha mtu au kitu kisichokuwepo. Kwa mfano kwenye muziki wa *Stick* maneno haya yametumika, *"Baby you know am out here working, I know you miss me…"*
Mwimbaji anawasiliana moja kwa moja na mpenzi wake ili kujenga uhusiano wa kihisia na mpenziwe na kuonyesha udharura. Kulingana na Wamitila (2003) mbinu hii hutumika kutilia mkazo maneno au jambo linalosemwa. Kwa mwimbaji, anasisitiza jinsi anavyochapa kazi na anavyompeza mwenzake. Inasababisha wasikilizaji au watazamaji wa wimbo huu kuwa na wakati wa ufaragha na mazungumzo ya kihisia ya kibinafsi.

**Taswira**
Hutumiwa kurejelea neno, kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani kwenye akili ya msomaji/msikilizaji na mtazamaji. Wimbo wa Stick umetumia kauli zifuatazo ambazo zimejenga taswira: *"Nakuja kuguza matit*, Am coming to give you the tongue, nakuja kaa nimemwag* ndan*."* Taswira hisi, oni na mwonjo zimejitokeza kwenye sentensi hizi na zinasawiri uhalisia wa kitendo cha jimai kwenye mawazo ya hadhira. Inaonyesha hali ya kufungamanishwa kimwili na kihisia kati ya hawa wawili japo kwa kutumia lugha chafu. Maneno haya yanaonyesha hali halisi ya maisha ya kisasa ya mijini.

**Misimu**
Kadhalika, kuna matumizi ya misimu ambayo ni lugha itumikayo kwa muda fulani halafu hutoweka. Neno mamaz (mama), ukaniseti (ukanianika), doo (pesa), m-fine (mzuri) mcute (mrembo) na seti, mtaa (nyumbani) keja (nyumba), nyege (hisia za mapenzi) na kaquickie (mapenzi ya dakika chache) ni misimu na aghalabu hupata mashiko katika mitaa ya nchi ya Kenya. Lugha hii hufanya wimbo kushabikiwa na kizazi cha vijana ambacho ndicho kinacholengwa.

Mbinu za kimtindo kama vile misimu, kuchanganya ndimi, taswira, jazanda, tadmini na ritifaa zimejenga uhalisia wa mazungumzo ya vijana wa mitaani katika nchi ya Kenya na jinsi ambavyo huelezea na kuonyesha hisia na matamanio yao. Uhalisia huu unakuwa mvuto kwa hadhira lengwa huku wimbo ukigusa hali halisi badala ya kitendo cha kuigizwa. Taswira inayojengwa na miziki hii inavuka mipaka ya kimaadili, inawafanya wanawake kusawiriwa kama vyombo vya kimapenzi na kuendeleza uchafu kwa hadhira. Hii inasababisha utovu wa maadili hasa kwa vijana. Ni wazi kuwa miziki hii miwili ina mbinu nyingi za kimtindo ila zinafaulisha maudhui ya utovu wa kimaadili. Zinasawiri uchafu unaotekelezwa kupitia kujamiana kwa hivyo hazifai kuchezwa.

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**
**Hitimisho:** Kutokana na utafiti uliofanywa, ni dhahiri kwamba miziki hii miwili inafaa kuchukuliwa hatua kali kama vile kudhibitiwa kwa misingi ya aliyoyatoa Plato kuhusiana na fasihi nzuri. Usaliti kwenye ndoa, ufuska, ukosefu wa uaminifu, kushabikia ulevi, ponografia, uchu wa ngono, tamaa ya pesa, uasherati, ubidhaishaji wa mapenzi na lugha mwiko ni maudhui yaliyojitokeza waziwazi kwenye miziki hii. Kadhalika picha na video zilizoko hazizingatii maadili. Kutokana na maoni aliyoyatoa Plato kuhusiana na fasihi nzuri, miziki hii imekosa kufikia kiwango cha kuitwa fasihi au sanaa nzuri. Inasisimua hisia na kuondoa urazini, inakosa ukweli kwa kutia chuku yanayoimbwa na itachangia



DRAFT

tabia mbaya kwa hadhira hasa vijana. Wasanii wanafaa vilevile wachukuliwe hatua kali za kisheria kwa ajili ya kutunga nyimbo ambazo zitafisidi jamii. Zaidi ya hayo, miziki hii miwili ikiendelea kuchezwa itajenga ukawaida wa matumizi ya lugha chafu katika usanii hasa miongoni mwa vijana.

**Mapendekezo:** Shirika la kudhibiti Miziki na filamu nchini Kenya linafaa kusisitiza umuhimu wa kumakinika zaidi kwa wasanii wanapotunga nyimbo ili kuhakikisha maudhui, video na picha zinazingatia maadili. Kadhalika, vituo vya mafunzo kama vile shule, vyuo vikuu na vyuo vya wanahabari vinafaa kuhusisha maadili ya kimziki na uwajibikaji katika ubunifu ili kuhakikisha yote yanayowasilishwa yana maadili. Tafiti za baadaye zinaweza kuchunguza mitandao mbalimbali ya kijamii inayotumika kama nyenzo ya burudani na kitega uchumi na jinsi maadili yanavyozingatiwa.

**MAREJELEO**


adelaja oriade. (2020). *Challenging hegemonic masculinity in nigerian hip hop*. Adelaja O. Oriade. https://www.academia.edu/69025184/Challenging_hegemonic_masculinity_in_nigerian_hip_hop

DJi KENYA. (2018, October 29). *Khaligraph Jones - Stick, Miti Freestyle [iXtendz] [2018]*. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=rAgfIT0_5HY

Kasyoka, E. N. (2022). *An analysis of "problematic contents" expressed in gengetone songs in Kenya.* https://erepository.uonbi.ac.ke/bitstreams/999af87e-e0f3-4b19-891e-26bbb00db00d/download

MAIN STREET. (2025, October 1). *Bahati - SETI (Official Audio)*. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=Rl8Dc_MF0Ng

Muchunku, I. G. (2023). Analyses of dynamics of censorship of music in East Africa: The case of Tanzania Communications Regulatory Authority and Kenya Film and Classification Board. *International Journal of Research and Innovation in Social Science, 7*(5), 517–541. https://doi.org/10.47772/IJRISS.2023.70543

Mutua, E. (2019). Public statement as CEO of the Kenya Film Classification Board regarding gengetone music. https://kfcb.go.ke/sites/default/files/2021-03/Takataka-16.4.19-8_0.pdf

Mutua, E. (2021). *Statement on immoral content in gengetone music*. Kenya Film Classification Board. https://shorturl.at/CjnFP

Ndiritu, N. N., Muchunku, I. G., & Mwikali, M. (2024). Socio-cultural dynamics in censorship of television advertisements in Kenya. *Journal of Innovation, Technology and Sustainability,* 2(1), 30–47. https://doi.org/10.70868/CFHE1584

Orodho, A. J., & Kombo, D. K. (2002). *Research methods: Qualitative and quantitative approaches*. Nairobi. https://usercontent.one/wp/ict-4mrpq.uccsri.com/wp-content/uploads/2025/12/ResearchMethodsManual_Final-EDITEDFFFF.pdf?media=1710763452

Snapes, L. (2019, February 14). *The greatest banned songs of all time – ranked!* The Guardian. https://www.theguardian.com/music/2019/feb/14/the-greatest-banned-songs-of-all-time-ranked

Stone, J. (2022). *The evolution of music censorship*. Daily Music Roll. https://www.dailymusicroll.com/entertainment/the-evolution-of-music-censorship.html

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya fasihi: Istilahi na nadharia*.